TANGAZO LA SERIKALI Na. 51N la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI WA KIHANDISI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA KIWANDA CHA KUTENGENEZA MABATI WA KAMPUNI YA LODHIA STEEL INDUSTRIES YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Huduma ya Ushauri Elekezi wa Kihandisi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Mabati wa Kampuni ya Lodhia Steel Industries ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 11 Oktoba, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Lodhia Steel Industries kwenye huduma za ushauri elekezi za kihandisi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Mabati inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2026 na kwa mujibu wa kipengele cha 3.3 cha mkataba wa utkelezaji baina ya Kampuni ya Lodhia Steel Industries na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31/12/2024

**MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
*Waziri wa Fedha*